



# ARUSHA MEAT CO. LTD

P. O. Box. 14167

ARUSHA – TANZANIA

+255 734 026 767

E-mail: arushameatcompany@yahoo.com

30/10/2024

## ZABUNI YA USAFI

1. Arusha meat Co.ltd kupitia kamati ya Manunuzi inakusudia kufanya mchakato wa Manunuzi kwa ajili ya kupata/ kuajiri kampuni ya usafi wa maofisini na mazingira yote kwa ujumla.

2. Meneja Mkuu wa Arusha Meat Co. Ltd kupitia Kamati ya manunuzi anatangaza Zabuni ya usafi kwa Kampuni zote za usafi zenye sifa na vigezo katika kazi tajwa wanaweza kupata taarifa kamili Ofisi ya Manunuzi Arusha Meat Co.Ltd na kutembelea eneo la kazi Arusha Meat co.ltd

### **Majukumu katika kazi ni kama ifuatayo;**

- a) Kufanya usafi katika vyoo na vyumba vya kubadilishia nguo.
- b) Kufanya usafi katika duka kuu la kampuni (SAKINA).
- c) Kufanya usafi wa mazingira yote ya kampuni.
- d) Kufyeka maeneo yote yaliyo ndani ya kampuni.
- e) Kutunza bustani zinazo zunguka ofisi za kampuni (Arusha meat co. ltd)

### **4. Sifa za kampuni ya Usafi inayotakiwa**

- i. Iwe na uzoefu usio pungua miaka miwili katika kazi kama ilivyo ainishwa hapo juu.
- ii. Iwe na namba ya uandikishaji wa mlipa kodi kutoka mamlaka ya mapato Tanzania (Tax Identification Number).
- iii. Iwe na mtaji wa kutosha kwa maana ya rasilimali watu na vitendea kazi muhimu.
- iv. Iwe na akaunti ya benki.
- v. Iwe na Leseni halali ya biashara.
- vi. Iwe na cheti halali cha usajili wa mahali pa kazi.

- vii. Iwe na orodha ya mikataba mitatu ya kazi ya usafi aliyopata hivi karibuni (2022/2023/2024) ikiwa ni pamoja na majina, mawasiliano na anwani za wateja kwa ajili ya kuthibitisha.
- viii. Taarifa ya fedha iliyokaguliwa angalau miaka miwili ya hivi karibuni.
- ix. Mamlaka ya wakili iliyothibitishwa kihalali (power of attorney).
- x. Taarifa ya akaunti ya benki ya miezi mitatu ya hivi karibuni.
- xi. Hati ya kukiri kufuata masharti ya kazi na uadilifu katika zabuni (Bid securing declatation).

**NOTE:**

- Maombi yanatakiwa yaambatanishwe na nakala za vivuli zilizo thaminishwa na wakili aliyesajiliwa na mamlaka husika.
- Wawakilishi wa Kampuni zote zilizoomba wawepo siku ya ufunguzi ili kufuatilia kwa ukaribu hatua zote za mchakato wa ufunguzi wa zabuni zilizowasilishwa
- Wazabuni wenye nia na uwezo wawasilishe maombi yao katika masijala kuu ya Arusha Meat Co. Ltd na kupewa utaratibu wa kukabidhi nyaraka (zabuni) zao.

Maombi yote yatumwe kupitia anuani ifuatayo:

Meneja Mkuu,  
Arusha Meat Co.Ltd,  
S.L.P. 14167,  
Arusha.

Maombi yote yafungwe ndani ya bahasha iliyofungwa kwa lakiri (seal) na juu ya bahasha iandikwe "Zabuni ya ulinzi Arusha Meat Company Ltd -**AMCL/TND/110/8**."

Mwisho wa kupokea zabuni ni tarehe **20/11/2024** saa nne kamili asubuhi (04:00 Asubuhi) na kufunguliwa tarehe **20/11/2024** saa nne na dakika moja asubuhi (04:01 Asubuhi) katika Ofisi za Arusha Meat Co. Ltd.

  
.....  
STEPHEN L SULTAN  
MENEJA MKUU  
ARUSHA MEAT COMPANY LTD  
